



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BENKI KUU YA TANZANIA



MPC Na.244

3 Julai 2026

Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha

1. Riba ya Benki Kuu

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC), ilifanya kikao tarehe 2 Julai 2026 na kuamua kuongeza Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 5.75 hadi asilimia 6.25 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2026. Uamuzi huu unalenga kudhibiti ongezeko la mfumuko wa bei unaotokana na kupanda kwa bei za mafuta, mbolea na gharama za usafirishaji, hali inayotokana na mgogoro unaoendelea Mashariki ya Kati.

Kamati imeona kuwa ongezeko hili la riba ni sahihi katika kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, na kuendelea kuchangia ukuaji wa shughuli za uchumi. Aidha, bei za chakula zinatarajiwa kupungua kufuatia mavuno mazuri ya msimu wa kilimo wa mwaka 2025/26. Vilevile, thamani ya shilingi inatarajiwa kuwa imara kutokana na mapato yatokanayo na mauzo nje ya nchi, ikiwemo dhahabu, mazao ya kilimo, na shughuli za utalii. Hali hii itasaidia kupunguza bei za chakula na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, na hivyo kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo katika nusu ya pili ya mwaka 2026.

2. Tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ilipungua katika robo mwaka iliyoishia Juni 2026, kutokana na kuongezeka kwa athari za mgogoro wa Mashariki ya Kati, ambao ulivuruga usambazaji wa mafuta na njia kuu za biashara. Mgogoro huu ulichangia ongezeko la bei za mafuta ghafi, mbolea, na gharama za usafirishaji. Mwenendo huu umesababisha mfumuko wa bei duniani kuanza kuongezeka na hivyo kudhoofisha matarajio ya ukuaji

wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2026. Mwelekeo wa uchumi wa dunia utategemea namna mgogoro wa Mashariki ya Kati utakavyoendelea.

3. Tathmini ya mwenendo wa uchumi wa ndani

Kamati ya Sera ya Fedha imeridhika na mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi, licha ya kuwepo kwa changamoto zilizotokana na mgogoro wa Mashariki ya Kati. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 6 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2026, ukichangiwa zaidi na ongezeko la uzalishaji katika shughuli za kilimo, ujenzi, madini, huduma za kifedha pamoja na usafirishaji. Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 6.6, ukichochewa zaidi na shughuli za utalii na ujenzi. Katika nusu ya pili ya mwaka 2026, uchumi unatarajiwa kuendelea kuwa imara, ukikua kwa zaidi ya asilimia 6.

Mfumuko wa bei umeendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5, licha ya kuongezeka kutokana na kupanda kwa bei za mafuta na gharama za usafirishaji duniani. Kwa upande wa Tanzania Bara, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 4.2 mwezi Mei 2026, kutoka asilimia 3.2 mwezi Machi 2026. Aidha, ruzuku ya mafuta iliyotolewa na Serikali mwezi Mei na Juni 2026 ilisaidia kupunguza kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 5.5 mwezi Mei 2026 kutoka asilimia 4.9 mwezi Machi 2026, ikilinganishwa na lengo la asilimia 5. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo, licha ya changamoto kutoka nje ya nchi.

Hali ya ukwasi katika robo ya pili ya mwaka 2026 ilikuwa sanjari na mwelekeo wa sera ya fedha. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa kasi ya kuridhisha ya wastani wa asilimia 24, ikichangiwa na ongezeko la mahitaji kutoka katika sekta za uzalishaji. Sekta ya kibenki iliendelea kutengeneza faida, ikiwa na mtaji wa kutosha kukabiliana na misukosuko ya muda mfupi. Aidha, ubora wa rasilimali uliendelea kuwa thabiti, kama inavyodhihirishwa na uwiano wa mikopo chechefu uliokuwa asilimia 2.9 mwezi Mei 2026, ikilinganishwa na kiwango kinachohimilika cha asilimia 5. Wakati huohuo, mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi na usalama.

Sekta ya nje ilikabiliwa na mtikisiko uliotokana na mgogoro wa Mashariki ya Kati, japokuwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilikuwa takriban asilimia 2.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka unaoishia Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 2.2 kwa mwaka ulioishia Machi 2026. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kuendelea kubaki katika kiwango hicho katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2026. Kwa upande wa Zanzibar, urari wa malipo uliendelea kuwa na ziada, ikichangiwa zaidi na mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha, ikifikia takriban dola za Marekani bilioni 6, kiwango kinachoweza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.3, juu ya lengo la nchi la angalau miezi minne. Akiba ya fedha za kigeni inatarajiwa kuongezeka, ikichangiwa na mauzo ya nje ya nchi na ununuzi wa dhahabu kutoka soko la ndani.

Utekelezaji wa sera ya bajeti uliendelea kuwa wa kuridhisha. Hii iliakisiwa na ongezeko la mapato ya kodi ambayo yalivuka malengo, pamoja na usimamizi mzuri wa matumizi na deni la Serikali. Katika mwaka 2025/26, mapato ya ndani yanakadiriwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 16.8 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 15.6 kwa mwaka ulipita.

4. Tarehe ya kutangaza riba mpya ya Benki Kuu

Kamati ya Sera ya Fedha itaendelea na dhamira yake ya kuhakikisha utulivu wa bei nchini. Kwa muktadha huu, Kamati itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa uchumi wa dunia na wa ndani pamoja na athari zinazoweza kuongeza mfumuko wa bei hapa nchini, ili kuchukua hatua stahiki pale inapohitajika. Kamati ya Sera ya Fedha inatarajia kukutana tena tarehe 7 Oktoba 2026, ambapo Riba ya Benki Kuu kwa robo ya nne ya mwaka 2026 itatangazwa siku inayofuata.


Emmanuel M. Tutuba
GAVANA